

CLASS 6 KISWAHILI END TERM 1 2020

Muda: Saa 1 Dak.40

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Mama ___ 1 ___ baba huitwa nyanya. ___ 2 ___ kawaida nyanya huwa mzee. Nyanya pia huitwa ___ 3 ___. Wazee ___ 4 ___ wanastahili kupewa heshima ___ 5 ___. Kinyume cha mzee ni ___ 6 ___. Watu wote wanastahili ___ 7 ___ ili ___ 8 ___ yote iwe na amani.

- | | | | |
|---------------------|--------------|-----------------|------------------|
| 1. A. wa | B. ya | C. cha | D. la |
| 2. A. Kuwa | B. Za | C. Na | D. Kwa |
| 3. A. babu | B. bibi | C. mama | D. shangazi |
| 4. A. zote | B. sote | C. yote | D. wote |
| 5. A. wao | B. chao | C. zao | D. lao |
| 6. A. msichana | B. kijana | C. mama | D. nyanya |
| 7. A. kudharauliana | B. kutwezana | C. kuheshimiana | D. kubembelezana |
| 8. A. jamii | B. jamaa | C. mbari | D. ukoo |


Sebuleni ___ 9 ___ palikuwa na ___ 10 ___ manne na vibago sita. Iiionekana ikiwa ___ 11 ___ kwa sababu ya zulia ___ 12 ___ lilikuwa jekundu. Dirishani palikuwa na ___ 13 ___ meupe pepepe. Wageni nao walikaribishwa na ___ 14 ___ wao kwa moyo ___ 15 ___.

- | | | | |
|----------------|------------|-------------|--------------|
| 9. A. yake | B. yao | C. mwao | D. pao |
| 10. A. makochi | B. meza | C. kabati | D. stuli |
| 11. A. mbovu | B. zuri | C. ovyo | D. maridadi |
| 12. A. ambao | B. ambayo | C. ambalo | D. ambacho |
| 13. A. masofa | B. mapazia | C. shubaka | D. matakia |
| 14. A. wenyeji | B. wageni | C. mahasimu | D. mashabiki |
| 15. A. msafi | B. chafu | C. mkunjufu | D. njema |

Kutoka nambari 16-30, jibu swali kulingana na maagizo.

16. Tegua kitendawili: Afuma lakini hana mishale.
- A. Nungunungu
B. Nzi
C. Ndege
D. Konokono

17. Umbo hili huitwaje ?



- A. Duaradufu
B. Mchemraba
C. Kopa
D. Mcheduara

CAT 003

1

KISWAHILI DARASA LA SITA

CLASS 6 KISWAHILI END TERM 1 2020

18. Kamilisha sentensi kwa kivumishi cha kumiliki.
Manukato _____ hunukia vizuri.
A. yale B. yako
C. yoyote D. mengi
19. Kanusha:
Mgeni hupikiwa uji wa wimbi.
A. Mgeni hatapikiwa uji wa wimbi.
B. Mgeni hakupikiwa uji wa wimbi.
C. Mgeni hapikiwa uji wa wimbi.
D. Mgeni hajapikiwa uji wa wimbi.
20. Salaale! Kumbe alipata ajali! Salaale ni neno la kuonyesha
A. kuridhika B. mshangao
C. kitendo D. kukataa
21. Tunasema yeye ananuka kama
A. beberu B. jeraha
C. choo D. fugo
22. Ndege ana manyoya lakini samaki ana
A. ngozi B. mapezi
C. magamba D. makacha
23. Kifaa kinachotumiwa na wachuuzi kupimia uzito ni
A. utepe B. mizani
C. pimamaji D. bisibisi
24. Neno **limbukeni** lina irabu ngapi tofauti ?
A. Tisa B. Tano
C. Nne D. Tatu
25. Jaza pengo:
Uzuri _____ unawavutia watu wote.
A. wenyewe B. yenyewe
C. ndiyo D. wenye
26. Kamilisha:
Safu ya _____
A. nyuki B. noti
C. milima D. pesa
27. Ni sentensi ipi sahihi kisarufi ?
A. Meza palipopanguswa ni safi.
B. Nyumbani mna watu wengi.
C. Uwanjani pale ni pasafi.
D. Darasani lile ni safi.
28. Ukisalimiwa "Alamsiki" utatoa jibu gani ?
A. Binuru B. Nawe pia
C. Salama D. Asante
29. Ushuri tano kwa tarakimu ni
A. $\frac{5}{9}$ B. $\frac{5}{6}$
C. $\frac{2}{5}$ D. $\frac{5}{10}$
30. Ni nini wingi wa :
Mbuzi alivunjika ubavu.
A. Mbuzi alivunjika mbavu.
B. Mbuzi walivunjika mbavu.
C. Mabuzi yalivunjika mbavu.
D. Mbuzi walivunjika ubavu.

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.

Mashairi ni mojawapo ya sanaa kubwa yenye maana iliyofichika. Wasanii wanaopata kutunga mashairi huitwa malenga. Nao wanaopenda kuyaimba na kuyakariri mashairi huitwa manju. Mashairi ni tungo zenye lugha nzuri iliyojaa utamu wa matamshi na mdundo. Lugha ya kishairi hutumia maneno haba. Maneno haya huhifadhi maana kamili kama alivyokusudia mshairi.

Mashairi kwa kawaida hugawanyika katika vifungu vinavyojulikana kama beti. Wingi au uchache wa beti hutegemea ujumbe wa mshairi. Mawazo na ujumbe ukiwa mzito, bila shaka beti huwa nyingi. Kwenye ubeti, hupatikana mshororo. Mshororo huwa sentensi za ubeti. Kila mshororo huwa na vitamkwa ambavyo huitwa mizani. Kwa kawaida mizani huwa kumi na sita katika kila mshororo.

CAT 003

2

KISWAHILI DARASA LA SITA

CLASS 6 KISWAHILI END TERM 1 2020

Mashairi nayo huwekwa katika makundi mbalimbali. Makundi haya huwa kulingana na idadi ya mishororo. Washairi wengi hupenda shairi aina ya tarbia. Hili ni shairi ambalo huwa na mishororo minne katika kila ubeti. Kuna bahari nyingine za mashairi kama tathlitha, takhmisa na tasdisa.

Mshairi huwa na kipawa ili atunge shairi. Huwa anaielewa lugha kwa mapana na marefu. Si mtu wa kuomba msamiati wa Kiswahili.

Mara nyingi mshairi anapoeleza jambo hutumia lugha kwa njia ya kipekee. Wakati mwingine mshairi hrefusha ama kufupisha idadi ya vitamkwa ili atimize idadi ya mizani. Hizi ni baadhi ya sheria za utunzi wa ushairi.

- | | |
|--|---|
| <p>31. Mtu anayetunga mashairi huitwaje ?
A. Msanii B. Malenga
C. Manju D. Mtunzi</p> <p>32. Ni kweli kusema kuwa mashairi
A. huchezwa B. huchukiza
C. hujengwa D. hukaririwa</p> <p>33. Bahari ya shairi hulingana na idadi ya
A. mizani B. wasanii
C. mishororo D. vitamkwa</p> <p>34. Beti nyingi za shairi huonyesha nini kulingana na kifungu hiki ?
A. Ujumbe mzito.
B. Mapenzi ya malenga.
C. Mawazo mepesi.
D. Manju na malenga.</p> <p>35. Mshororo nusu wa ubeti huwa na mizani mingapi ?
A. Kumi na sita B. Minne
C. Minane D. Kumi</p> <p>36. Maana iliyofichika ni sawa na
A. maana bayana.
B. jambo linaloonekana.
C. maana ya ajabu.
D. maana isiyo wazi.</p> | <p>37. Wasanii wengi hupenda kutunga mashairi gani ?
A. Ya mishororo minne.
B. Yenye mdundo.
C. Ya tathlitha.
D. Yenye beti nne.</p> <p>38. Ili mshairi atunge shairi zuri, ni sharti
A. awe na marefu na mapana.
B. aelewe lugha barabara.
C. aelewe lugha zote.
D. asiwe na kipawa.</p> <p>39. Kulingana na aya ya mwisho ni kweli kusema kuwa
A. mshairi hutumia nomino za pekee.
B. washairi wote hufanana.
C. mshairi hafupishi maneno sana.
D. ushairi una sheria zake.</p> <p>40. Malenga huwa stadi wa lugha kwa sababu gani ?
A. Huomba maneno mengine.
B. Anauelewa msamiati.
C. Huburudisha watu.
D. Hutunga shairi na nyimbo.</p> |
|--|---|

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.

Ilikuwa siku ya Jumamosi. Kwa kuwa sikuwa nikienda shule, ilikuwa siku yangu ya kupumzika. Kwa kuwa nilitamani sana kuona vitu vile watu huona wakivua samaki, nilimshawishi babangu ili aniruhusu tuwe pamoja. Aliniuliza maswali chungu nzima. Baadaye aliitikia twende pamoja. Kwa mara ya kwanza, ningepanda mashua na kusafiri pamoja na abu yangu.

Tulipanda mashua na **kung'oa nanga**. Mara tu tulipoanza kuvua, kukawa na wingu jeusi tititi.

CAT 003

3

KISWAHILI DARASA LA SITA

CLASS 6 KISWAHILI END TERM 1 2020

Mvua na dhoruba kubwa ilianza na upepo wa kila namna ulivuma. Hapo nilipatwa na woga wa kunguru. Nilikodoa macho na kumkaribia baba yangu.

Bahari ilichafuka tukawa hatuoni mbele wala nyuma. Wale wote waliokuwa mashuani walitapatapa kama kuku aliyenusurika kunyakuliwa na mwewe. Mimi nilipigwa na butwa na kuanza kutafakari hatima yetu. Kila mtu alikuwa hajijui hajitambui.

Nilipomwangalia babangu alikuwa na wasiwasi wa mwasi. Aliniangalia kwa huruma na kusema, "Nilikukanya kuja lakini ukanikaidi. Ona sasa. Utafanyaje?" Nilimkodolea macho na kumwomba msamaha. Kila mtu alianza kumwomba Mola kwani Mungu kasema niombe nikupe.

Iwapo siku ile ilikuwa ya mauko, tulikuwa tayari kuabiri gari la kwenda peponi.

Wasiwasi wetu uliisha wakati upepo uliacha kuvuma na kukawa shwari. Kila mtu alishusha pumzi na kumshukuru Mungu wake. Tulipata wasamaria wema na kutuvuta hadi ufuoni. Nilimshukuru Mola kwa kutuokoa.

- | | |
|---|--|
| <p>41. Msimulizi alitaka kwenda kuvua kwa kuwa
A. alikuwa mvuvi hodari.
B. alipenda kula samaki.
C. alikuwa mpenda raha.
D. ilikuwa siku ya kupumzika.</p> <p>42. Msimulizi aliwezaje kwenda na babaye ?
A. Alimshawishi B. Alimghilibu
C. Alimbeza D. Alimhonga</p> <p>43. Ni kweli kusema kuwa
A. msimulizi alipenda sana kuvua.
B. babaye msimulizi alipenda kuwa mvivu.
C. watu wengi hawakupenda kuvua.
D. msimulizi alipanda mashua siku hiyo.</p> <p>44. Ni nini maana ya kung'oa nanga ?
A. Kuenda safari.
B. Kuanza safari.
C. Kufika tamati.
D. Kuwa wa mwisho.</p> <p>45. Msimulizi alimkaribia baba yake kwa sababu
A. ya woga.
B. ya wasiwasi.
C. ya ukakamavu.
D. ya ujasiri.</p> | <p>46. Unafikiri ni kwa nini watu hawakuwa hawajijui hawajitambui ?
A. Kulikuwa na mvua.
B. Walikuwa wameaga.
C. Walikuwa na jakamoyo.
D. Kulikuwa na giza.</p> <p>47. Wasafiri wote walikuwa tayari kufa kwa sababu
A. wasingeweza kujiokoa.
B. mashua yao ilijaa maji.
C. walikosa msamaria mwema.
D. walikuwa na woga.</p> <p>48. Wasiwasi iliisha punde tu wakati
A. wasafiri walipona.
B. wasafiri waliaga.
C. bahari ilipoa.
D. upepo uliongezeka.</p> <p>49. Wasafiri walifika aje ufuoni ?
A. Waliogelea. B. Walisaidiwa.
C. Walitembea. D. Walijisaidia.</p> <p>50. Kichwa mwafaka cha kifungu hiki ni
A. Uvuvi na bahari.
B. Samaki wa baharini.
C. Upepo mwanana baharini.
D. Safari ya baharini.</p> |
|---|--|